

MAKAO MAKUU

Ghorofa ya 4, Jengo la LAPF, Barabara ya Makole
S.L.P. 2857, Dodoma, Tanzania
Simu: +255-26 2329002-3; Nukushi: +255-26 2329005
Barua pepe: info@ewura.go.tz Tovuti: <http://www.ewura.go.tz>

TAARIFA KWA UMMA

UFAFANUZI KUHUSU UPOTOSHWAJI WA BEI ZA MAFUTA

1. UTANGULIZI

Moja ya majukumu ya Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) katika kudhibiti sekta ndogo ya mafuta ni pamoja na kushamirisha ushindani kwa kuweka mizania sawa ya ushindani; na kumlinda mtumiaji wa huduma.

Katika kutimiza jukumu hili, EWURA hukokotoa bei kikomo za mafuta kwa nchi nzima ikizingatia gharama halisi za uagizaji wa mafuta ambazo hujumuisha bei ya mafuta katika soko la dunia, gharama za usafirishaji, kodi na tozo mbalimbali za serikali, faida ya wafanyabiashara na gharama za usafirishaji ndani ya nchi.

Kwa sasa mafuta yanapokelewa katika Bandari za Dar es Salam, Tanga na Mtwara, hivyo kuchochea uwepo wa tofauti za bei kikomo. Bei hizo kikomo hutangazwa kila Jumatano ya kwanza ya mwezi kwa kutumia kanuni maalum (**Petroleum Pricing Setting Rules**) iliyopitishwa kwa mujibu washeria.

Kwa mujibu wa kanuni hiyo, ukokotozi wa bei kikomo ya mafuta kwa mwezi husika hapa nchini, huzingatia bei ya mafuta katika soko la dunia iliyopo katika mkataba wa kuingiza mafuta, kwa meli zote zilizopakua mafuta mwezi mmoja kabla ya kutangazwa kwa bei kikomo; na kawaida, wastani wa bei ya mafuta ya soko la dunia ya miezi miwili nyuma kabla ya kutangazwa kwa bei kikomo ya mafuta.

Kwa Mfano, bei za mafuta hapa nchini kwa mwezi Agosti 2018 zitakotolewa kwa kuzingatia mafuta yaliyopakuliwa mwezi Julai, 2018 na bei za mafuta katika soko la dunia za mwezi Juni 2018; ambazo ndizo ziko katika mikataba ya kuingiza mafuta hayo nchini.

2. KIINI CHA TOFAUTI ZA BEI YA MAFUTA KATI YA DAR ES SALAAM NA TANGA KWA MWEZI JULAI 2018

Bei za mafuta kwa mwezi Julai 2018 zimeonekana kuwa na tofauti kubwa kati ya mafuta yaliyoingizwa nchini kupitia bandari ya Dar es Salaam na ile ya Tanga. Tofauti hiyo ya bei inatokana na sababu mbalalimbali kama zilivyoelezwa hapa chini:-

(a) Meli sita kati ya saba za mafuta ya Petroli na Dizeli zilibeba mafuta yenye gharama za mwezi Mei 2018, katika soko la dunia; na zilipakua shehena hiyo bandari ya Dar es Salaam mwezi Juni 2018. Bei hizo za soko la dunia ndizo zilizotumika kukokotoa bei za mafuta ya soko la ndani kwa mwezi Julai, 2018.

Kimsingi bei ya mafuta ya soko la dunia ya mwezi Mei 2018 ilikuwa juu ikilinganishwa na ile ya mwezi Machi 2018, ambayo ilitumika kukokotoa bei za mafuta kwa soko la ndani kwa mwezi Juni 2018.

(b) Tofauti na Dar es Salaam, hakuna meli iliyopakua mafuta katika bandari ya Tanga kwa mwezi Juni 2018. Bandari ya Tanga ilipokea meli ya mafuta kwa mara ya mwisho **mwezi Aprili 2018, ambapo mafuta hayo yalikuwa na bei ya soko la dunia ya mwezi Machi 2018**; iliyokuwa pungufu ikilinganishwa na bei ya mafuta ya mwezi Mei 2018, katika soko la dunia.

Aidha, meli hii ilikamilisha kupakua mafuta katika bandari ya Tanga mwezi Mei 2018, na bei za mafuta hayo zilianza kutumika mwezi Juni 2018 ambazo zimeendelea kutumika hadi mwezi Julai 2018 kwa kuwa hakuna meli ya mafuta iliyopokelewa katika bandari ya Tanga kwa mwezi Juni, 2018.

3. ONYO:

EWURA inatoa ONYO kali kwa wote wanaosambaza habari za kupotoshwa kwa suala hili kwani kinachofanyika ni kutaka kuvuruga soko hatua ambayo inaweza kutafsiriwa kama uhujumu uchumi. Hivyo basi atakayebainika atachukuliwa hatua kali za kisheria.

IMETOLEWA NA:

Idara ya Mawasiliano na Uhusiano

Julai 30, 2018

Dodoma.